



# UCSAF yaifungua Zanzibar kupitia uboreshaji wa huduma za mawasiliano

Jafari Juma, Mwananchi

Zanzibar imeshuhudia ukuaji wa sekta ya mawasiliano ambayo katika kipindi cha miaka mitatu umechangia katika kuboresha maisha ya wananchi kijamii na kiuchumi sambamba na pato la Taifa.

Ukuaji wa sekta hiyo umechangiwa na kuwepo kwa sera, sheria, kanuni na mfumo mzuri wa utaji leseni za huduma za mawasiliano pamoja na usambazaji wa huduma za mawasiliano kwenye maeneo mbalimbali.

Sekta hii inachangia katika uchumi moja kwa moja na kwa kupitia sekta za utalii, elimu, afya, kilimo, biashara, ajira, fedha, uwekezaji na sekta nyingine zote kama nyenzo ya uwekezaji katika kuongeza ufansi wa utendaji kupitia jamii habari. Ukuaji imara wa sekta ya mawasiliano ni sehemu ya matunda yanayotokana na juhudi za dhati za Serikali, sekta binafsi na wadau.

Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imekuwa ikifanya juhudi kuhakikisha sekta ya mawasiliano inakuwa na kumnufaisha kila Mzanzibar.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia UCSAF kwa kushirikiana na kampuni ya simu za mkono ni MIC (TIGO) iliweza kujenga jumla ya minara 42 Zanzibar ikiwa ni muendelezo wa kuboresha huduma za mawasiliano hususani katika kuunga mkono jitihada za Rais Dk Samia Suluhu pamoja na Rais Dk Hussein Mwinyi katika kutangaza utalii.

Utekelezaji wa miradi wa kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo hayo 42 ulikamilika na kuzinduliwa Oktoba 26, 2022 na Dk Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Aidha kupitia mradi huu, wananchi 211,601 wa visiwa vya Pemba na Unguja wanunufaiwa na huduma za mawasiliano kutoka kampuni ya simu ya MIC (Tigo) ambapo kwa sasa wanaweza kuwasiliana na ndugu zao, kupata huduma za kifedha kupitia mitandao ya simu.

Aidha baada ya kukamilika kwa mradi huu ambao kwa kiasi kikubwa kumetatu



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Ali Mwinyi akizindua moja kati ya minara 42 ya mawasiliano ya simu liyojengwa kupitia ruzuku inayotolewa na UCSAF.

**Sh 6.9 bilioni**

Fedha zilizotumika katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa minara 42 Zanzibar ambapo ni ruzuku kutoka serikalini.

**211,601**

Idadi ya wananchi wanaunufaiwa na mradi wa ujenzi wa minara 42 Unguja na Pemba.

**2022**

Mwaka ambao mradi wa ujenzi wa minara 42 Zanzibar ulizinduliwa na Rais Dk Hussein Mwinyi.

changamoto ya mawasiliano ya simu kwa wananchi wa visiwa vya Pemba na Unguja ambapo sasa wananchi hao wanunufaiwa na huduma ya mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kufanya biashara ya kuuza vocha, kufungua vibanda vya kutoa huduma za miamala ya kifedha pamoja na masuala mengine ya kijamii.

Mradi huu ulitekelezwa kwa ruzuku ya Serikali inayotolewa na UCSAF ambapo kiasi cha Sh 6.9 bilioni kilitengwa kutekeleza mradi huo huku maeneo 42



Moja kati ya minara 42 ya mawasiliano ya simu Zanzibar iliyojengwa kupitia ruzuku inayotolewa na UCSAF.

ya Unguja na Pemba yakunufaiwa na mradi huo.

Mbali na miradi hiyo, UCSAF kwa kushirikiana na Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation (MIF), Zanzibar wamepeleka vifaa

vya TEHAMA kwenye Skuli nne za Sekondari pamoja na kufanya ukarabati wa maabara za kompyuta na uwekaji wa miundombinu ya intaneti.

Shule za sekondari zili-

zonufaiwa na mkakati huo ni pamoja na; Kizimkazi Dimbani, Kizimkazi Shehia ya Mkunguni, John Pombe Magufuli na Hasnuu Makame.

Hii imetokana na kuka-

milika kwa mradi wa ujenzi wa minara ya mawasiliano ambao umefungua fursa za matumizi wa TEHAMA kwenye sekta mbalimbali Zanzibar.